# INGHAM
# Early Learning Calendar



# JINSI YA KUTUMIA KALENDA HII



Kujifunza huanza wakati wa kuzaliwa! Ni muhimu kwa familia wote kujisikia kama wanasaidiwa na kujua jinsi ya kuwahimiza watoto utotoni mwao. Kalenda hii ilitengenezwa ili kukupa baadhi ya maelezo na mwongozo kuhusu jinsi unaweza kuwasaidia watoto kujifunza na kujiandaa kufanikiwa katika shule ya watoto wadogo.

Kalenda hii ina maelezo mbalimbali yanayohusiana na kuwaandaa watoto kufanikiwa katika shule ya watoto wadogo, yale watoto watakuwa wakijifunza katika shule ya watotowadogo na mambo ya kufurahisha mnayoweza kufanya pamoja kuanzia kuzaliwa ili kukuza na kutegemeza ujuzi wa watoto!

- Shughuli za kila siku zinaweza kutumika kulingana na umri wa mtoto wako, mapendekezo au kiwango cha ujuzi.
- Kalenda hii imeundwa ili kutumiwa katika mwaka wowote. Visanduku tupu vinaweza kuachwa wazi, kutumika kupiga tiki kwenye shughuli zilizokamilishwa, au kuandika tarehe.
- Kila mwezi huangazia rasilimali ya ndani ambayo familia yako inaweza kutaka kutumia au kutembelea.
- ***Hatua za Maendeleo*** na dhana za ***Kujifunza Mahali Popote*** zinaweza kupatikana nyuma ya kalenda.

Watoto hujifunza ujuzi mwingi tofauti katika maeneo yafuatayo ambayo yatawasaidia kuwa tayari kufanikiwa katika shule ya watoto wadogo. Kila siku ya wiki huzingatia eneo tofauti.

## **Jumapili:** Ukuzaji wa Lugha

Shughuli zitamsaidia mtoto wako kujifunza ujuzi huu:

- Kujibu maswali kuhusu hadithi mliyosoma pamoja.
- Kuweza kushiriki mara mbili au zaidi katika mazungumzo.
- Kutumia maneno aliyojifunza kutoka kwa hadithi, uzoefu na mazungumzo.
- Watu wengi kuweza kukuelewa.
- Kutumia mimi, yeye na yake vizuri.

## **Jumatatu:** Ukuzaji wa uwezo wa Kusoma na Kuandika

Shughuli zitamsaidia mtoto wako kujifunza ujuzi huu:

- Kucheza na sauti katika maneno (kutia vina, sauti za mwanzo).
- Kutambua herufi kubwa 18 na herufi ndogo 15 na sauti zinazotoa.
- Kugundua jina lao lililoandikwa.
- Kuangalia kitabu kuanzia mbele hadi nyuma na kupindua kurasa moja baada ya nyingine.
- Kuandika jina lao la kwanza kuanzia herufi kubwa na kumalizia na herufi ndogo.

## **Jumanne:** Ukuzaji wa Hesabu

Shughuli zitamsaidia mtoto wako kujifunza ujuzi huu:

- Kuhesabu kwa sauti hadi 20.
- Kuhesabu vitu 10 kwa usahihi.
- Kutambua nambari 1-20.
- Kutambua maumbo msingi (mraba, mviringo, pembetatu, n.k.).
- Kuunda mpangilio wa sehemu mbili (kijani, nyeupe, kijani, nyeupe).
- Kupanga vitu kulingana na kitu vinavyoshirikiana kwa pamoja (rangi, ukubwa, umbo, n.k.)

## **Jumatano:** Kukua Kimwili

Shughuli zitamsaidia mtoto wako kujifunza ujuzi huu:

- Kuruka kwa miguu miwili.
- Kudumisha nafasi ya kibinafsi ya watu wengine.
- Kutumia mshiko (kidole gumba na vidole viwili) kuandika au kuchora herufi, nambari au umbo.
- Kutumia makasi ya watoto.

## **Alhamisi:** Kukua Kijamii

Shughuli zitamsaidia mtoto wako kujifunza ujuzi huu:

- Kuwaamini watu wazima na watoto wengine.
- Kucheza na, si kando tu, na watoto wengine.
- Kujifunza na kushiriki katika kikundi.

## **Ijumaa:** Kukua Kihisia

Shughuli zitamsaidia mtoto wako kujifunza ujuzi huu:

- Kuwa mbali na mlezi msingi kwa kipindi kirefu.
- Kushughulikia mahitaji yao ya kibinafsi (k.m. kunawa na kujipanguza baada ya kwenda choo, kunawa mikono).
- Kudhibiti maonyesho ya hisia zao.

## **Jumamosi:** Njia za Kujifunza

Shughuli zitamsaidia mtoto wako kujifunza ujuzi huu:

- Kuonyesha tamaa na msukumo wa kujifunza vitu vipya.
- Kutumia dakika 10-15 kushughulikia kazi zinazomvutia.
- Kulenga na kuzingatia shughuli moja kwa dakika 10-15.
- Kukumbuka na kuunganisha uzoefu na mazingira (dukani, maktaba).
- Kufuata maelekezo ya hatua mbili na kukumbuka taratibu za kawaida.
- Kufuatilia na kutatua matatizo rahisi.



# KUCHEZA NI KUJIFUNZA

Kucheza ni kazi ya watoto. Huleta furaha, hutoa nguvu, na huwapa watoto njia ya kujionyesha. Pia kucheza huhimiza ubunifu, uwezo wa kufikiria, kujiamini na uwezo wa kutatua matatizo. Usiwahi kamwe kuacha kucheza pamoja!

- **WATOTO WACHANGA:** huchunguza na kucheza kwa kuweka vitu midomoni mwao na kuvigonganisha sakafuni. Kuwa mwangalifu kuhusu hatari ya vitu vinavyokaba koo. Vitu ambavyo vinaweza kupitia tyubu ya karatasi ya choo vinaweza kuwa hatari ya kuwapalia watoto wachanga.
- **WATOTO WADOGO:** huiga vitendo na tabia za wengine. Wanajifunza huruma na kushirikiana kupitia michezo.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** wana uwezo wa kuwa makini zaidi na uwezo wa kuzingatia. Toa muda wa kutosha kwa watoto kushiriki katika shughuli zao wazipendazo za kucheza.

# JANUARI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Makundi ya Michezo na Masomo hutoa shughuli kwa familia kucheza na kuchunguza pamoja na watoto wao wenye umri wa miaka minne na chini. Makundi hutolewa katika maeneo mbalimbali katika eneo la huduma la Ingham. Tembelea *www.inghamgreatstart.org* au ratiba ya sasa ya Kundi la Michezo na Masomo.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Imba wimbo wa alfabeti. | **A** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore " **A**" mkiwa pamoja. Tafuta "**A**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /a/ kama vile *andazi*. | Umbo la leo ni **pembetatu**. Angalia ni **pembetatu** ngapi unazoweza kupata. | Cheza densi, densi, densi! Washa muziki na mcheze densi na mtoto wako. | Kuwa mkarimu zaidi kwa mtu leo. | Himiza mtoto wako kujilisha wakati wa kula. | Tengeneza mtu wa theluji. |
| Ongea na mtoto wako kuhusu supu aipendayo mtoto wako. | **B** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore "**B**" mkiwa pamoja. Tafuta "**B**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /b/ kama vile *bata*. | Rangi ya leo ni **bluu**. Angalia ni vitu vingapi vya **bluu** unavyoweza kuvipata leo. | Toka nje na mtengeneza malaika wa theluji pamoja. | Tembelea sehemu ya watoto ya maktaba ya eneo lako. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. Tembelea tovuti ya maktaba yetu kwenye *www.cadl.org* au *www.elpl.org*. | Chora uso wenye furaha na uzungumzie mambo ambayo yanakufurahisha. | Kata vipande vya theluji kutoka kwenye karatasi na mzipambe mkiwa pamoja. |
| Jifunzeni neno jipya mkiwa pamoja na mjizoeze kulitumia. | Someni kwa pamoja kitabu mnachokijua. Kisha mruhusu mtoto wako "kukusomea" hadithi. | Leo tunashughulikia nambari **1**. Angalia ni "**1**" ngapi unazoweza kupata unapokuwa ukiendelea na shughuli zako za siku. | Nendeni nje na beleshi mkiwa pamoja. | Panga tarehe ya kucheza na binamu, jirani au rafiki. | Himiza mtoto wako kufanya usafi mwenyewe baada ya kula. | Nyumbani, igiza hadithi ya *Sungura na Kobe* kwa kutumia wanyama sesere. |
| Imba wimbo wako upendako kwa mtoto wako. Uliza mtoto wako ni wimbo upi anaoupenda sana. | **C** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore "**C**" mkiwa pamoja. Tafuta "**C**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /c/ kama vile *chai*. | Hesabu ni mbogamboga ngapi unazokula siku. Zina rangi gani. | Chora maumbo katikamchanga. Kutambua maumbo ni mwanzo wa kutambua herufi na nambari. | Kaa chini na kula pamoja. Mweleze mtoto wako kuhusu siku yako na muulize ameshindaje. | Jifunze kunawa mikono, kusugua meno na kuchana nywele mkiimba "Maua mazuri yapendeza.. | Ongea na mtoto wako kuhusu wakati walikuwa wachanga. Ni mambo gani waliyoyafanya na kusema. |
| Imba "Maua mazuri yapendeza." Onyesha baadhi ya ishara za mkono kulingana na wimbo/ vina. | Kusoma kabla ya kulala ni utamaduni unaoheshimika. Ni wakati upi unaweza kupata kusoma na mtoto wako? Jaribu muda wa kuoga, wa kula, muda wa kwenda choo, na miadi ya daktari. | Hesabu vidole vya mikono na miguu vya mtoto wako. | Tumia vitu vya kawaida vya nyumbani kutengeneza vizuio. Kwa mfano, mito ya viti, foronya, kikapu cha nguo za kufua. | Chezeni mchezo kwa pamoja kama vile Ruka ruka ruka simama kaa. | Msaidie mtoto wako kufikiria kuhusu kitu anachoweza kumfanyia mtu mwingine. | Ongea kuhusu nyenzo tofauti: karatasi, kitambaa, mbao, chuma, n.k. Je, unaweza kutafuta vitu vilivyoundwa na vitu hivi. |

## WIMBO/VINA:
## Maua Mazuri Yapendeza

Maua Mazuri yapendeza
Ukiyatazama.
Yanayomeremeta.
Ukiyatazama, yanayomeremeta.
Maua Mazuri Yapendeza.



# MUZIKI NI WA KILA MTU

Kwa kweli muziki ni wa kila mtu! Mtoto wako angependa kusikia sauti yako haijalishi unavyoimba.

- **WATOTO WACHANGA:** hufurahia nyimbo, kucheza na vidole na kucheza densi. Shughuli hizi zinatuliza na kufurahisha, na huleta hisia ya usalama na kuondoa dhiki.
- **WATOTO WADOGO:** huitikia muziki kwa kusonga na kucheza. Kwa kusonga, watoto wadogo huipa nguvu misuli yao kubwa na kujifunza ushirikiano.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** hupata ujuzi wa kusoma na kuandika kupitia muziki. Nyimbo, mashairi na vina huwasaidia watoto kugundua sauti za nyimbo na kujifunza kuzingatia vina, ambayo ni ujuzi muhimu wa kabla ya kusoma.

# FEBRUARI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Jiji la East Lansing hufadhili maonyesho ya moja kwa moja ya muziki kwa familia kama sehemu ya Mfululizo wa Tamasha za Watoto BILA MALIPO. Tafuta ratiba ya sasa ya Mfululizo wa Tamasha za Watoto kwenye *www.cityofeastlansing.com/137/Childrens-Concert-Series*.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Tengenezeni mapishi pamoja. Zungumzia kuhusu jinsi chakula kinavyonukia, kuonekana, na ladha yake itakuwaje. | **D** ndio herufi ya siku. Fuatisheni/ mchore "**D**" mkiwa pamoja. Tafuta "**D**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /d/ kama vile *dudu*. | **Mraba** ndio umbo la leo. Hesabu ni miraba mingapi unazoweza kupata leo. | Ruka juu, ruka chini, ruka kama chura. | Tembelea sehemu ya watoto ya maktaba ya eneo lako. | Msaidie mtoto wako kumpigia simu mtu maalum ili kumwambia vitu 2 anavyopenda kuhusu yule. | Nenda matembezi ya nje wiki hii! Je, msimu wa baridi huwa unaonaje katika mtaa wako? |
| Unda orodha ya watu maalum na uzungumzie kuhusu ni nini huwafanya kuwa maalum. | Zungumzia kuhusu sehemu za kitabu: kichwa, mwandishi, mchora picha na mwelekeo tunaotumia kusoma. | Rangi ya leo ni **nyekundu**. Angalia ni vitu vingapi **nyekundu** unavyoweza kupata. | Chagua mmoja wa watu wako maalum na mwandikie mtu huyo barua kwa pamoja. | Wasilisha barua hiyo mlioandika kwa mtu huyo wako maalum. | Zoea kuwa msafi: kutoa makamasi kwa kutumia tishu, kukohoa na kupiga chafya kwenye mkono, kunawa mikono na kutupa tishu. | Kamilisheni chemsha bongo pamoja. |
| Zungumzia kuhusu vitu vyako vyote uvipendavyo. | **E** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore "**E**" mkiwa pamoja. Tafuta "**E**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /e/ kama vile *embe*. | Leo tunashughulikia nambari **2**. Angalia ni **2** ngapi unazoweza kupata. | Jifunze kuruka kwa mguu mmoja, kisha ule mwingine. Hesabu jinsi unavyoruka. Piga makofi kwa kila mruko. | Jiunge na Kundi la Michezo na Mafunzo. Ili kutafuta eneo liliko karibu na kwako, tembelea *www.inghamgreatstart.org*. | Nawa mikono na umweleze kwa hatua sahihi. Tunga wimbo kuhusu kunawa mikono. | Tengeneza kitabu cha hali ya hewa kwa kutumia karatasi. Chora picha za aina tofauti za hali ya hewa na uzizungumzie. |
| Zungumzia kuhusu siku ya mtoto wako. Mweleze atakachokuwa akifanya, k.m. kula, kulala, kwenda dukani. Huu huongezea misamiati yake ya kila siku. Muulize anafikiria ni nini kitakachomfurahisha sana. | Angalia kitabu cha picha na uelezee hadithi bila kutumia maneno. Vitabu vya picha visivyokuwa na maneno vinapendekeza na kukuza lugha! | Changanya vyombo vyako vyote vya jikoni na umruhusu mtoto wako avipange kwa njia tofauti. Kupanga ni njia nzuri ya ustadi wa mapema wa hesabu. | Igiza wimbo wa, "Kichwa Bega, Goti na Kidole." | Panga tarehe ya kucheza na binamu, jirani au rafiki. | Vaa nguo **nyekundu** leo. | Cheza mchezo wa kusikiliza/kufuatilia kama vile "Simon Anasema" na mtoto wako. |
| Katika sehemu ya mazao ya mboga dukani, taja rangi zote unazoweza kuona. | Tengeneza mabango yenye maneno ya ufafanuzi kama vile "moto", "laini", n.k. na uyabandike nyumbani pote. | Hesabu soksi nyumbani mwako zilizo kivyake na katika jozi. Zungumzia vitu vinavyokuja kwa jozi. | Kata mioyo. Weka sakafuni. Ruka kwa miguu miwili kutoka moyo mmoja hadi mwingine. | Kaa chini na kula pamoja. Zungumzia kuhusu shughuli yako uipendayo katika majira ya baridi. | Soma hadithi na mtoto wako. Mwambie aeleze/ achore/aandike ni nini alichokipenda kuhusu kitabu. | Tengeneza orodha ya kanuni za usalama za familia yako. Zungumzia kuhusu ni kwa nini unahitaji kuwa na kanuni. |

**WIMBO/VINA:**
**Kichwa Bega, Goti na Kidole**

*(Ukiimbwa kwa tuni ke. Wakati wote, gusa sehemu ya mwili wako ambayo inayolingana na wimbo.)*
**Kichwa bega goti na kidole, goti na kidole.**
**Kichwa bega goti na kidole, goti na kidole, macho, masikio, mdomo, na pua.**
**Kichwa bega goti na kidole.**



# KUSOMA NA MTOTO WAKO

Kujifunza kusoma na kuandika huanza wakati wa kuzaliwa! Kuwasomea vitabu watoto kwa sauti ni mojawapo ya shughuli muhimu zaidi katika kuendeleza ufahamu na ustadi unaohitaji kwa ufanisi wa kusoma baadaye.

- **WATOTO WACHANGA:** hujifunza kuongea kwa kusikiliza maneno yanayozungumzwa. Vitabu vya bodi ni chaguo nzuri kwa watoto - ni ndogo, imara na vina kurasa ambazo ni rahisi kupindua. Pia watoto wanapenda kuona nyuso, kwa hivyo tafuta vitabu vyenye picha za watu wenye umri wote.
- **WATOTO WADOGO:** Washirikishe watoto wadogo kwa kutumia vitabu vyenye vina, mwendo, mifuatano na kuimba. Watoto wadogo hujifunza kupitia kurudia na wanaweza kuomba kitabu au mchezo ule mmoja tena na tena.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** wako tayari kusikiliza hadithi ndefu, lakini usisahau kuzifanya za kufurahisha na za kutangamana. Picha zenye aina nyingi za maneno zitakuza misamiati na ufahamu wa dhana mpya.

# MACHI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Ushirikiano wa Kusoma na Kuandika wa Masomo ya Utotoni (The Early Childhood Literacy Coalition) husheherekea uwezo wa kusoma na kuandika na wiki mbili za shughuli bila malipo na sherehe ya kuweza kusoma na kuandika mapema kila mwezi Machi. Tafuta ratiba kamili kwenye tovuti ya Maktaba ya Wilaya ya Capital Area kwenye *www.cadl.org*. Tafuta ukurasa wa facebook wa ECLC kwenye *www.facebook.com/EarlyChildhoodLiteracyCoalition.*

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zungumzia kuhusu ruwaza. Je, ni wanyama gani wenye mistari? Ni wagani wenye madoa? | **F** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore "**F**" kwa pamoja. Tafuta "**F**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /f/ kama vile *fisi*. | **Mstatili** ndio umbo la leo. Hesabu ni **mistatili** mingapi unayoweza kupata. | Cheza muziki na densi. | Panga tarehe ya kucheza na binamu, jirani au rafiki. | Jifunze kuvaa na kuvua nguo za nje. | Onyesha mtoto wako jinsi ya kupima kwa kutumia vikombe vya kupimia. Waruhusu wajifunze kwa kutumia maji na maharagwe kavu. |
| Mruhusu mtoto wako kuandaa chakula au kitafunio. Zungumzia kile ambacho wewe na mtoto wako mnachokifanya. | Zungumzia kuhusu silabi kama sauti katika maneno. Piga makofi kwa baadhi ya maneno kwa pamoja. Piga makofi mara moja kwa kila silabi au fungu la maneno. | Rangi ya leo ni **zambarau**. Angalia ni vitu vingapi vya **zambarau** unavyoweza kupata leo. | Watoto wanapenda kusaidia! Mpe mtoto wako kitambaa kidogo ili aweze kupanguza pamoja na wewe. | Tembelea maktaba. | Chora uso wenye huzuni. Elezea kuhusu wakati ulihisi huzuni. | Kusanya vitu 3 vya **zambarau** katika nyumba yako. Zungumzia kuhusu aina za rangi. Je, ni gani yenye giza/ang'avu zaidi? |
| Anza kila siku kwenye dirisha na uzungumzie kuhusu hali ya hewa. | **G** ndio herufi ya siku. Fuatisheni/ mchore "**G**" kwa pamoja. Tafuta "**G** au vitu vinavyoanza na sauti ya /g/ kama vile *gari*. | Leo tunashughulikia nambari **3**. Angalia ni "**3**" ngapi unazoweza kupata unapokuwa ukiendelea na shughuli zako za siku. | Tengeneza ngome na msome ndani yake pamoja. | Kaa chini na kula pamoja. | Panga vitu vya kuchezea vingi kama uwezavyo ndani ya sekunde 30. | Kusanya vitu vya ajabu na uviweke ndani ya mfuko. Mfanye mtoto wako ahisi kitu kwenye mfuko na akisie ni nini. |
| Sema na uige mchezo wa, "Ulingo Bayoyo." | Kwa sababu ya burudani tu, soma kwa kutumia tochi. Tengeneza vikaragosi vya kivuli au msimuliane hadithi. | Vaa nguo ya **zambarau** leo. | Tafuteni **mstatili** nyumbani, mkisonga kama wanyama tofauti kutoka chumba kimoja hadi kingine. | Jifunze kutumia "Tafadhali" na "Asante" na watu wengine. | Zungumzia kuhusu unavyohisi wakati theluji inapoyeyuka. | Mchezo wa unamu: mpe mtoto wako vipande vya karatasi, vitambaa, na kadibodi. Zungumzia kuhusu unamu tofauti. |
| Dukani la mboga, zungumzia kuhusu vitu ambavyo ni baridi. | Tengeneza kitabu chako mwenyewe. Unganisha karatasi pamoja. Mtoto huchora picha na wazazi huandika maneno. | Hesabu milango na madirisha yote katika nyumba yako. Je, kuna milango na madirisha zaidi? | Tengeneza kitu kutoka kwa sanduku la kadibodi na utepe. | Nendeni pamoja kutembelea bustani/uwanja wa kucheza katika eneo lako. | Saidia kuondoa vitu mezani na kuosha vyombo. | Zungumzia kuhusu utamu, chumvi, chungu, pilipili, na chachu. Onja kitu na ujadili alichokipenda zaidi. |

## KUCHEZA NA VIDOLE: Ulingo Bayoyo

**Ulingo Bayoyo**
**Dada/Kaka kasie ingie kati tukuone**
**Maringo yako abingilibingili!** *(acheze kati kati kwa ubunifu)*
**Mpaka chini!** *(peperusha mkono wa kulia nyuma ya mgongo)*
**Come back, Jack!** *(peperusha mkono wa kushoto nyuma kutoka kwa mgongo wako)*
**Come back, Jill!** *(peperusha mkono wa kulia nyuma kutoka kwa mgongo wako)*



# SAYANSI KILA SIKU

Sayansi iko kila mahali—kuanzia wanyama, mimea na viumbe vyote, hadi afya na lishe, hadi zana na mashine, na zaidi! Watoto kwa kawaida huwa na hamu kuhusu ulimwengu wao na sayansi hutia moyo upendo wao wa uchunguzi.

- **WATOTO WACHANGA:** hujifunza kuhusu ulimwengu na sifa za vitu kwa kutumia hisia zao zote. Wanapoangusha kitu cha kuchezea na unakichukua, wanajifunza kuhusu sababu na matokeo.
- **WATOTO WADOGO:** wanajaribu kujua jinsi ulimwengu unavyofanya kazi. Kwa kuwa wanapokuwa wakitumia hisia zao tano wanaendelea kufahamu ulimwengu wao. Mtie moyo mtoto wako kujaribu vitu. Je, ni nini kitakachofanyika ukiweka kijiti ndani ya kidimbwi cha matope? Mtoto wako anapokuwa akiangalia kwa karibu vitu vya asilia, vipe jina vitu hivyo vilivyopatikana.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** hutumia majaribio na makosa, sehemu muhimu ya mchakato wa sayansi. Watu wazima wanaweza kutia moyo hamu kwa kuuliza maswali na kuwaruhusu watoto kuchunguza njia nyingi tofauti zinazowezekana.

  Unafikiria hiyo hufanya kazi kivipi?
  Je, ni kwa nini unafikiria twiga zina shingo ndefu?
  Je, ni zana gani itatusaidia kufanya kazi hii?
  Je, ni nini itafanyikia kipande hiki cha barafu tunapoweka ndani ya maji moto?

# APRILI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Tamasha la Sayansi la MSU ni mfuatano wa hafla ya ajabu kwa siku kadhaa ambayo huangazia nyanja za sayansi, teknolojia, uhandisi, sanaa na hesabu (STEAM). Kwa ratiba kamili ya mwaka huu tembelea *www.sciencefestival.msu.edu.*

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Imba na uige "Little Bo Peep." | Imba wimbo wa alfabeti. | Leo tunashughulikia nambari **4**. Fikiria vitu **4** ambavyo ni vizito. Fikiria vitu **4** vilivyo ufukoni. | Chagua vyakula 3 vipya na uwe na jaribio la familia kuonja. | Uliza mtoto wako kama unaweza kujiunga katika mchezo wake. Hii huiga jinsi ya kujiunga na wengine wakati wa kucheza. | Paka rangi picha unapokuwa ukisikiliza muziki. Zungumzia kuhusu ulivyohisi. | Kata picha katika vipande ili kutengeneza chemsha bongo , kisha viweke tena pamoja. |
| Tunga wimbo kuhusu sehemu ya mpangilio wa kila siku wa mtoto wako. | **H** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/mchore "**H**" kwa pamoja. Tafuta "**H**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /h/ kama vile *hema.* | Rangi ya leo ni **kijani**. Angalia ni vitu vingapi vya **kijani** unavyoweza kupata. | Weka vizuizi vya mtoto wako kupita juu, chini ndani, nje, kuzunguka na katikati. | Soma kitabu kuhusu urafiki na ongea kuhusu jinsi ya kuwa rafiki mzuri. | Tafuta mahali patulivu nyumbani mwako. Mtie moyo mtoto wako kutembelea mahali hapa wakati anahitaji kutulia. | Onyesha mtoto ni wakati gani kwa siku ni wakati wa kiamsha kinywa, chakula cha mchana, na chakula cha jioni. Zungumzia kuhusu taratibu zipi hufanyika kwa wakati gani. |
| Omba mtoto wako abashiri ni nini kitakachofanyika katika kitabu kwa kuangalia jalada. | "Piga rangi" ya mistari, miviringo au herufi kwenye barabara ndogo kwa kutumai maji. | Rukeni pamoja na mhesabu kwa sauti. Angalia mnawezaje kuhesabu zaidi kwa pamoja! | Kunja soksi ili kutengeneza mpira. Vuta kikapu cha nguo za kufuliwa na utupe mpira huo wa soksi ndani yake. Songa nyuma kila wakati. | Uliza mtoto wako kama unaweza kutumia kitu chake cha kuchezea akimaliza kucheza nacho. Msaidie kufuatilia baada ya mtoto wako kumaliza. | Mpe mtoto wako kikapu cha kujaza vitu ambavyo mtoto wako anavipenda. Zungumzia kuhusu vitu alivyokusanya. | Zungumzia kuhusu machaguo na mtoto wako. Hakikisha kumpa machaguo mara nyingi kama uwezavyo. |
| Rudia sauti ambazo mtoto wako anazitoa kwa mtoto wako. | Mfanye mtoto wako atafute na kuweka mduara kwenye herufi zote kwenye furushi la nafaka au furushi zingine za nafaka. | **Mduara** ndio umbo la leo. Hesabu ni **miduara** mingapi unayoweza kupata leo! | Cheza mchezo wa kusimama tuli. Cheza muziki kwenye simu yako na mcheze densi pamoja. Wakati mziki unapokoma, nyote msimame tuli. | Nenda kwenye kituo cha ununuzi na mcheze na watoto wengine katika eneo la kuchezea. | Fanyeni nyuso tofauti mbele ya kioo pamoja. Zungumzia kuhusu hisia. | Wakati moto wako anapokuuliza swali, muonyeshe jinsi ulivyopata jibu kwenye kitabu au tovuti. |
| Cheza mchezo wa mkahawa na mtoto wako. Mchezo wa kujifanya hukuza misamiati! | **I** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/mchore "**I**" mkiwa pamoja. Tafuta "**I** au vitu vinavyoanza na sauti ya /i/ kama vile *iliki.* | Pikeni pamoja! Mtie moyo mtoto wako kutumia vikombe vya kupigia kupima na kuongezea viambatano. | Tengenezeni unga wa kuchezea mkiwa pamoja (kikombe 1 cha unga wa ngano + kikombe ½ cha chumvi + karibu kikombe ½ cha maji) na utumie mikono yako kutengeneza vitu tofauti. | Chora picha au tengeneza kadi kwa jirani yako na uiwasilishe. | Tafuta nyuso zenye furaha katika vitabu, kisha nyuso zenye huzuni. Zungumzia kuhusu hisia. | Pata baadhi ya nyenzo zilizotengenezwa upya (kadibodi, kontena za plastiki, n.k.) na uziunganishe. Tengenezeni kitu mkiwa pamoja leo! |

**VINA:**
**Little Bo Peep**

Little Bo-Peep has lost her sheep,
And can't tell where to find them.
Leave them alone and they'll come home,
Wagging their tails behind them.



# HISIA ZA KUTANGAMANA

Huenda mtoto wako anajifunza jinsi ya kutangamana katika mpangilio wa kikundi. Anajifunza matarajio yako, jinsi ya kutangamana na watoto wengine na kukuza ufahamu wa kanuni. Pia anaanza kukuza uwezo wa kudhibiti hisia zake. Na msaada kutoka kwako, watoto hujifunza ujuzi huu.

- **WATOTO WACHANGA:** Kuunga mkono ukuaji wa hisia za kutangamana humaanisha kutimiza mahitaji yao. Kuwajibu wanapokuzungumzia, kujibu wanapolia, na kuwaruhusu kuchunguza ulimwengu wao ukiwa karibu.
- **WATOTO WADOGO:** Watoto wadogo wanapokuwa wakiyapitia hisia zao, ipe hisia hizo majina. Fuata maelekezo ya mtoto wako wakati wa kucheza. Wasaidie wanapokuwa wakitaka kucheza na watu wengine. Jaribu kutoa nyenzo mbalimbali, ili kila mtoto mdogo awe na yake.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** Unga mkono vivutio vya mtoto wako wa chekechea katika kucheza na watoto wengine. Uliza maswali kama vile "hiyo inaweza kukufanya uhisiaje?" ili kusaidia kukuza huruma na ufahamu wa mtazamo. Mruhusu ajue unatambua wakati anafanya kitu cha msaada.

# MEI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Utafiti unaonyesha kwamba watoto wanaohudhuria mipango ya hali ya juu ya shule ya CHEKECHEA wana uwezo zaidi wa:

- Kusoma vizuri kabla ya darasa la 3
- Kuhitimu kutoka shule ya sekondari
- Kwenda chuo kikuu
- Kupata kipato cha juu zaidi

Watoto wengi wa umri wa miaka mitatu na nne wanastahiki shule ya CHEKECHEA isiyolipishwa karo. Ili kujifunza mengi kuhusu machaguo na kukamilisha maombi (hatua ya kwanza katika mchakato wa kuunganishwa na mpango), nenda kwenye *www.inghampreschool.org* au piga simu 1-855-644-7735.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Tumia soksi kama kikaragosi ili kuigiza "Eentsy Weentsy Spider." | Hudhuria muda wa hadithi wa maktaba ya eneo lako. Toa kitabu. *www.cadl.org/events* au *www.elpl.org*. | **Almasi** ndio umbo la leo. Hesabu ni **almasi** ngapi unaweza kupata leo. | Kwa kutumia vishikilio vyako vya jikoni, jifunze kusogeza vitu kutoka bakuli moja hadi nyingine. | Tengeneza chemsha bongo kwa kukata mbele ya boksi ya nafaka zilizoandaliwa (sirioli). Irejeshe pamoja ukiwa na mtoto wako kwa kubadilishana katika kuweka kila kipande. | Weka kioo kidogo mbele ya macho ya mtoto wako. Fanya nyuso tofauti mbele ya kioo. | Fanya mpango wa kesho na mtoto wako. Uandike. Ufuatilie. |
| Panua lugha ya mtoto wako. Wakati mtoto wako anaposema "Viatu vyangu," unaweza kusema "Hivyo ni viatu vyako vyekundu vinavyong'aa." | **J** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore "**J**" kwa pamoja. Tafuta "**J**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /j/ kama vile *jua*. | Nenda ukatembee na ukusanye vitu vya kawaida (mawe, misonobari, n.k). Chora unachokipata. | Rukeni pamoja na mhesabu kwa sauti. Angalia mnawezaje kuhesabu zaidi kwa pamoja! | Jifunze kujibu na "Sijambo" wakati mtu anapokusalimia. | Soma kitabu kuhusu hisia. Nenda kwenye maktaba yako na uulize mwangalizi wako wa maktaba kwa dhana za vitabu. | Zungumzia kuhusu safari ya familia ya hivi karibuni. |
| Wakati unasoma kitabu, uliza mtoto wako kubashiri ni nini kitakachofanyika kabla ya kupindua ukurasa wa mwisho. | Ukiwa na mtoto wako, tafuta herufi ya kwanza katika jina la mtoto wako katika maeneo mengi kama iwezekanavyo. | Leo tunashughulikia nambari **5**. Tafuta vitu **5** vidogo. Tafuta vitu **5** vikubwa. Tafuta vitu **5** vyenye ukubwa wastani. | Weka muziki na mcheze pamoja! | Jifunze kusema "tafadhali" na "asante" kwa Kihispania. "Por Favor" y "Gracias." Jifunze na watu unaowaona. | Soma kitabu kuhusu urafiki na ongea kuhusu jinsi ya kuwa rafiki mzuri. | Mwisho wa siku angazia kitu ambacho kilikufanya uhisi furaha. Uliza mtoto wako kuangazia ni nini kilichomfurahisha. |
| Kwa kutumia simu yako, piga picha ya mambo ya asili katika maeneo ya kushangaza (mpasuo barabarani). Onyesha picha na uulize mtoto wako kukusimulia hadithi. | Mfanye mtoto wako aandike orodha ya mahitaji na akusaidie kupata vitu ukiwa dukani. | Weka chumvi, mchanga, au krimu ya kunyolea kwenye bamba ya biskuti. Chora maumbo kwenye nyenzo. Mfanye mtoto wako ataje umbo hilo. Sasa ni zamu yako. | Mfunze mtoto wako kunawa mikono yake—juu, katikati na kati ya vidole—kwa muda wote wa wimbo wa Heri ya Siku ya Kuzaliwa. | Leo ni siku ya **waridi**. Angalia ni vitu vingapi vya **waridi** unavyoweza kupata Zungumzia ni vitu vingapi ni vya **waridi**. | Piga picha za uso wa mtoto wako akionyesha furaha, huzuni, uwoga, wasiwasi... Zichapishe picha hizo kwenye kioo chake. | Tambua wakati mtoto wako anapotatua tatizo lake mwenyewe. Mweleze mtoto wako na uorodheshe njia ambazo alitatua tatizo hilo. |
| Tafuta mfuko na uweke baadhi ya vitu anavyovijua ndani yake. Tafuta na ufafanue kitu. Mfanye mtoto wako akisie kitu hicho ni nini. Sasa ni wakati wako wa kukisia! | **K** ndio herufi ya siku. Fuatisheni/ mchore "**K**" kwa pamoja. Tafuta "**K**" au vitu ambavyo vinaanza na sauti ya /k/ kama vile *kakakuona*. | Chukua maua mtaani mwako na uzibane katikati ya kurasa za kitabu kikubwa. Hesabu petali na majani. | Cheza mpira mkiwa na mtoto wako. | Cheza kidimbwini na rafiki. Ona ni nani anayeweza kurusha maji zaidi! | Lala mgongoni nje na utazame mawingu. Zungumzia kuhusu wanyama anaowapenda. | Mfanye mtoto wako akusaidie kufua nguo, kulinganisha soksi na kupanga vitu. |

## WIMBO: The Eentsy Weentsy Spider

The eentsy weentsy spider climbed up the water spout.
Down came the rain and washed the spider out.
Out came the sun and dried up all the rain and the
Eentsy weentsy spider climbed up the spout again.



# KUCHEZA NJE

Kumbuka ukicheza nje ukiwa mtoto, hisia ya uhuru na kustaajabisha? Kucheza nje huwasaidia watoto kukua kimwili kwa kutumia misuli mikubwa kukimbia na kuruka. Kujifunza huboreshwa mtoto anapokuwa akijifunza mitazamo, sauti, harufu na unamu mpya. Watoto wa umri wote wanahitaji kutoka nje, wakati wa majira ya machipuko, joto, majani kupukutika na baridi.

- **WATOTO WACHANGA:** hunufaika na kutembezwa nje kwa kutumia kitembezaji, ambapo wanasikia kelele za nje, kuona mwangaza na upepo halisi, na wanaanza kufahamu hisi ya kwenda nje. Kukaa kwenye manyasi hutoa mchango wa unamu na harufu tofauti.
- **WATOTO WADOGO:** wanapenda uzoefu mpya wa kuwa nje, na watajifunza ujuzi mpya. Kutembea kwenye maeneo na miteremko tofauti huwezesha misuli yao kujifunza njia mpya za kusaidia miili yao.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** hufurahia mambo mapya nje—ndege na chindi, mawingu, vijiti na mawe. Wanaweza kutumia vitu hivi kuunda au kutumia kwa njia tofauti. Ni fursa ya kukimbia, kuruka na kucheza kwa njia ambazo ni tofauti na kuwa ndani.

# JUNI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Vituo vya mambo ya asili ni rasilimali nzuri za kucheza na kujifunza nje. Kaunti ya Ingham inajivunia vituo vitatu vyenye vijia, matukio na fursai nyingi za elimu—Fenner Nature Center, *www.mynaturecenter.org* Harris Nature Center, *www.meridian.mi.us* chini ya Parks and Recreation Woldumar Nature Center, *www.woldumar.org*.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Soma kitabu kuhusu wanyama na utoe baadhi ya sauti za wanyama. | Onyesha mtoto wako kwamba kuna vitu vya kusoma kila mahali. Tengeneza mchezo wa kutafuta vitu vyenye maneno (kama mikopo ya supu na maboksi ya nafaka zilizoandaliwa). | Leo ni siku ya rangi ya **machungwa**. Angalia ni vitu vingapi vya rangi ya machungwa unavyoweza kupata. Zungumzia kuhusu ni vitu vingapi vina rangi ya **machungwa**. | Imba "Kichwa, Bega, Goti na Kidole" ukionyesha misogeo. Sasa imba kwa kutumia sehemu nyingine za mwili. | Tembelea bustani ya eneo lako. Jifunze kucheza na watoto wengine. | Iga mbinu za kutulia (kupumua polepole, kufinya mto, n.k.) Zitumie kabla ujaribu kutatua tatizo. | Mpe mtoto wako vitu 15 tofauti kutoka kwenye droo iliyo nyumbani mwako. Angalia ni njia ngapi zinaweza kupangwa. |
| Soma na uigize "Mzinga ." | Kwa pamoja, orodhesha maneno mengi yenye vina na neno "nyuki". | Leo tunashughulikia nambari **6**. Angalia ni **6** ngapi unazoweza kupata unapokuwa ukiendelea na shughuli zako za siku. | Cheza "Fuata Kiongozi" na usonge kwa njia tofauti: kutembea, kuruka, kutambaa, kuruka kwa mguu mmoja. | Alika rafiki aje wacheze. Tengenezeni mchezo mpya kwa pamoja. | Msaidie mtoto wako kufikiria kuhusu kitu anachoweza kumfanyia mtu mwingine. | Jifanye unaenda safari ya kupiga kambi. Kusanya vitu utakavyohitaji na andaa kambi! |
| Tafuta sauti za vitu unavyofahamu kwenye simu yako kama vile treni, mbwa akibweka au honi ya gari. Zichezee mtoto wako, na umruhusu akisie ni sauti za nini. | **L** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore "**L**" kwa pamoja. Tafuta "**L**" ai vitu vinavyoanza na sauti ya /l/ kama vile *lugha.* | Kuelea au Kuzama? Tafuta vitu nyumbani mwako. Pata bakuli ya maji. Mfanye mtoto wako akisie kama vitaelea au kuzama. Ijaribu. Panga vitu kulingana na vile vinavyoelea na vinavyozama. | Jifunze kutumia vifungo na zipu kwenye nguo au sesere. | Mwandikie barua rafiki au ndugu. | Uliza mtoto wako ni nini hufanya mtoto wako kuhisi furaha. Piga picha ya mtoto wako akihisi furaha akifanya anachofurahia kufanya. Anzisha kitabu cha hisia. | Unda mfuko wa siri kwa mtoto wako. Weka kitu kimoja ndani ya mfuko na mpe ishara za maneno kuhusu utambulisho wa kilicho ndani. Mruhusu mtoto wako kuhisi, kuelezea, na kukisia ni nini kilichomo kabla ya kuangalia. (rudia) |
| Soma kitabu kwa kutumia picha pekee. | Nendeni kukusanya vijiti. Tumia vijiti hivyo kuunda herufi. | Umbo la yai ndio umbo la leo. Hesabu ni umbo la yai ngapi unaweza kupata leo! | Kata umbo la yai kutoka kwa aina tofauti za karatasi (gazeti, msasa, karatasi ya nta, n.k.). Je, ni gani ni kubwa? Ni gani ni laini? | Tembelea maktaba ukiwa na mtoto wako wiki hii. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. Tembelea matukio: *www.cadl.org/events* au *www.elpl.org*. | Zungumzia kuhusu jinsi sisi sote ni wa kipekee na maalum. Mfanye mtoto wako ataje baadhi ya mambo maalum kuhusu wao wenyewe. | Nenda kusaka mawingu. Tandaza blanketi ardhini na uone ni vitu gani unaweza "kupata" mawinguni. (wanyama, maumbo, n,k.) |
| Nenda kwa matembezi ya kusikiliza! Omba mtoto wako asikilize na aelezee sauti anazozisikia. | **M** ndio herufi ya siku. Fuatisheni/ mchore "**M**" kwa pamoja. Tafuta "**M**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /m/ kama vile *mamba.* | Unda ruwaza kwa kupiga makofi na kugonga. Mfanye mtoto wako afuate ruwaza yako. Sasa fuata ya kwake. | Jifunze kusonga kama wanyama tofauti. Tambaa kama mamba, telezateleza kama nyoka, ruka kama sungura, simama bila kuyumba kwa mguu mmoja kama bata aliyepumzika. | Nendeni kusaka mambo ya asili na rafiki. Tafuta rangi na unamu tofauti na uone ni vitu ngapi ya rangi ya kijani utakazopata. | Kata picha kutoka kwa magazeti zinazoonyesha hisia tofauti. Chagua picha na uige unachoweza kufanya ikiwa utahisi hivyo. | Zungumzia kuhusu maumbo tofauti na sehemu za gari. Je, unaweza kuchora gari kwa pamoja? |

## KUCHEZA NA VIDOLE:
## Mzinga

*(Funga mikono pamoja ili kutengeneza mzinga.)*
Hii ni mzinga. / Nyuki wako wapi?
Wamefichwa mbali mahali hakuna mtu anaweza kuwaona. *(Angalia mzinga kwa karibu.)*
Hivi punde watatoka nje ya mzinga.
Moja, mbili, tatu, nne, tano! *(Ondoa vidole kulingana na hesabu yako.)*
Bzzzzzzz! *(Tenganisha mikono; peperusha vidole kana kwamba ni nyuki.)*

# LISHE NA MTOTO WAKO ANAYEKUA



Lishe nzuri huwapa watoto nguvu na vitamini wanazohitaji ili kujifunza na kukua. Kujifunza tabia nzuri za kula ukiwa mtoto ni muhimu kwa maisha mazuri ya usoni.

- **WATOTO WACHANGA:** wanahitaji virutubisho na vitamini zinazopatikana katika maziwa ya mama au fomula ya watoto wachanga. Daktari wako wa watoto anaweza kupendekeza kuanzisha nafaka ya watoto wachanga na mbogamboga na matunda rojo baada ya umri wa miezi sita.
- **WATOTO WADOGO:** huchagua sana wanachokila, lakini hao hujifunza kwa kuwatazama wengine. Kula vyakula mbalimbali na mtoto wako atakuwa na uwezo zaidi wa kujaribu vyakula vipya pia. Mpe vipande vidogo vya matunda na mbogamboga kila wakati wa chakula.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** wanaweza kusaidia kupanga baadhi ya sehemu za chakula zao. Wape machaguo mawili—kama vile brokoli au karoti—na mwache mtoto wako aamue. Fanya chakula kuwa wakati wa familia na mzungumzie kuhusu kuchagua vyakula vya afya.

# JULAI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Tembelea soko la wakulima la eneo lako ili kununua mazao mabichi kwa ajili ya familia yako. Tembelea Masoko ya Wakulima ya Eneo Kuu la Lansing kwenye *www.lansing.org* kwa orodha ya masoko yaliyopo karibu na kwako.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Angalia picha za familia kwa pamoja. Fafanua msamiati kama vile "familia", "babu/bibi," "mjomba/baba mkubwa/ mdogo," n.k. | **N** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore **N** kwa pamoja. Tafuta "**N**" au vitu ambavyo vinaanza na sauti ya /n/ kama vile *nyuki*. | Tengeneza mteremko: pamba mwisho mmoja wa bodi au kitu kingine kikubwa tambarare. Jaribu jinsi vitu tofauti "vinateremka" kwenye mteremko. | Kata pembetatu zenye ukubwa tofauti kutoka kwenye karatasi au kitambaa. Je, ni gani ni kubwa? Ni gani ni laini? | Tengeneza mwaliko wa rafiki aje ili kucheza. | Mweleze mtoto wako wakati ambao ulijivunia na kisha umwambie akueleze wakati alijivunia. | Tengeneza mapishi ya kujifanya mkiwa nje. Sema, "ni nini tunapaswa kuweka ndani ya supu hiyo?" na mpatie mtoto wako jiwe la "viazi." |
| Panua mazungumzo ya mtoto wako. Wakati mtoto wako anapayuka/kuongea jibu kwa kusema: "Oh hilo ni wazo nzuri!" au "Ni nini hufuatia?" | Unda herufi kwa kutumia mawe na vijiti vilivyo nje. | Leo ni siku ya **manjano**. Angalia ni vitu vingapi vya **manjano** unavyoweza kupata. Zungumzia kuhusu vitu ambavyo ni vya **manjano**. | Chora kwenye kijia cha kutembea kwa kutumia chaki. Tengeneza barabara kwa magari ya kuchezea. | Tembelea maktaba ukiwa na mtoto wako wiki hii. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. Tembelea matukio ya maktaba: *www.cadl.org* au *www.elpl.org*. | Fikiriakitu ambacho unaweza kufanya kumsaidia mtu leo. | Tengeneza unga wa kuchezea nyumbani (kikombe 1 cha unga wa ngano kikombe + ½ cha chungaumvi + karibu kikombe ½ cha maji). Changanya pamoja. Ongezea harufu kwa kutumia viungo au kuongezea rangi ya chakula. |
| Zungumzia kuhusu maumbile ya mtoto wako. Sema, "Macho yako, yako wapi? Oh, ndio haya hapa." Omba watoto wakubwa waonyeshe sehemu za mwili wao. | **O** ndio herufi ya siku. Fuatisheni/ mchore **O** pamoja. Tafuta "**O**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /o/ kama vile *onja*. | Leo tunashughulikia nambari **7**. Angalia ni "**7**" unazoweza kupata unapokuwa ukiendelea na shughuli zako za siku. | Cheza mpira na mtoto wako. Kaa sakafuni mkiangaliana na mbiringize mpira. | Nenda kwenye bustani ya eneo lako na ujifunze kubadilishana zamu kwenye mtelezo. | Zungumzia kuhusu jinsi unavyohisi siku yenye joto. | Tambua maeneo unapokuwa ukiyapita ukiendesha gari. Sema unakoenda na unachokifanya na mtoto wako. |
| Nenda kutembea nje na usikilize. Tambua sauti unazosikia. | Tengeneza maneno ya upuuzi yenye vina. Tengeneza ufafanuzi wa kujifanya pia! | **Pembetatu** ndio umbo la leo. Hesabu ni **pembetatu** ngapi unazoweza kupata leo! | Weka muziki na mcheze densi na mtoto wako. Jaribu aina tofauti za densi na mtingize miili yenu! | Kaa chini na kula pamoja, zungumzia kuhusu shughuli yako uipendayo ya msimu wa joto. | Soma kitabu na mtoto wako na mwambie akueleze jinsi hadithi hiyo inamfanya ahisi. | Tengeneza chemsha bongo kutoka kwenye picha (gazeti, boksi ya nafaka zilizoandaliwa (sirioli), n.k.) na uzipange kwa pamoja. |
| Imba na uigize "Five Green and Speckled Frogs." | Msaidie mtoto wako kuandika jina lake kwenye kibodi. | Zungumzia kuhusu vinyume leo (kubwa, ndogo; fupi, ndefu; n.k.) Tafuta mifano ya vinyume mahali popote uendapo! | Kuwa chura chenye madoa, ruka ruka kwenye chumba ukiimba wimbo huo. | Alika rafiki yako kucheza majini. | Jifunze kusugua meno kwa pamoja kama familia. | Cheza "I Spy" nje. |

## WIMBO: Five Green and Speckled Frogs

Five green and speckled frogs sat on a hollow log
Eating some most delicious bugs. Yum, yum!
One jumped into the pool where it was nice and cool
Then there were four speckled frogs.
*(Rudia kwa kutumia chura nne, kisha tatu, na kuendelea.)*



# KUKUA KIMWILI

Misuli mikubwa na midogo ya watoto inakua na ku ka kila siku. Watoto hujifunza kazi za kimwili kwa viwango tofauti lakini katika mpangilio unaoweza kubashiriwa.

- **WATOTO WACHANGA:** wanaweza kuinua vichwa vyao karibu miezi mitatu, baadaye watainua kifua, kisha kubiringiza, kutambaa, kukaa, kusimama na mwishowe kujifunza kutembea. Hakikisha mtoto wako ana eneo salama na safi ambapo anaweza kupata muda kulala kifudifudi kila siku.
- **WATOTO WADOGO:** wanapenda kusonga. Mpe mtoto wako nafasi ya kukimbia, kupanda, na kutupa vitu katika maeneo salama. Mpe shughuli za kuimarisha mkono/mshiko wake, kama vile kutumia kijiko, kuchana karatasi, na kupindua kitasa cha mlango.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** wanapaswa kujifunza kukimbia, kuruka kwa miguu yao miwili, kuruka na kwenda mbio. Mpe mtoto wako nafasi nyingi za kutumia krayoni, penseli na makasi ya watoto.

# AGOSTI

**RASILIMALI ZA NDANI:** Kuna bustani nyingi za ndani ambazo hutoa maeneo ya kucheza kwa watoto wenye umri tofauti. Tembelea Bustani za Kaunti ya Ingham kwenye *www.pk.ingham.org*. Pia tafuta Maonyesho ya Afya ya Kurejea Shuleni yanayofadhiliwa na Idara ya Afya ya Kaunti ya Ingham kwenye *www.hd.ingham.org/ForParents.aspx*.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfanye mtoto wako akupe maelekezo ya kuvaa nguo au kutengeneza kitafunio. Kosea na umruhusu akukosoe! | **P** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/mchore **P** kwa pamoja. Tafuta "**P**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /p/ kama vile *panya*. | Leo tunashughulikia nambari **8**. Angalia ni "**8**" unazoweza kupata unapokuwa ukiendelea na shughuli zako za siku. | Tengeneza mistari kwa kutumia chokaa au kamba na ujifunze kutembea bila kuyumbayumba. | Tatua chemsha bongo au cheza mchezo pamoja. Jifunze kubadilishana zamu! | Jiunge na kundi la michezo na mafunzo. Nenda kwenye *www.inghamgreatstart.org* ili kutafuta eneo liliko karibu na kwako. | Cheza na sufuria yenye maji na vikombe, vijiko na bakuli za plastiki. |
| Jifanye kama unaongea kwa simu na mtoto wako. Jifunze kupokea simu na kumwalika mtu aje kucheza. | Andika jina la mtoto wako. Mfanye afuatilie herufi kwa kutumia kidole chake na kisha na kalamu. | Kusanya mfuko wenye vitu kutoka nje, kisha vipange kulingana na vitu vinavyoshirikiana pamoja. | Jifunze kukata miraba kwa kutumia makasi. | Alika jirani, rafiki au ndugu kwa siku ya kucheza. | Imba "Kama Unafuraha na Unajua Piga Makofi!" Tengeneza mistari ya ziada! | Tengeneza unga wa wingu kuchezea kwa pamoja (kikombe ¼ cha mafuta + vikombe 2 vya unga wa ngano). Mruhusu mtoto wako kucheza na vitu hivi nje kwenye nyasi! |
| Sema na uige mchezo wa vidole wa "Five Plump Peas." | **Q** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/mchore **Q** mkiwa pamoja. Tafuta "**Q**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /q/ kama vile *quit*. | **Mraba** ndio umbo la leo. Hesabu ni **miraba** mingapi unazoweza kupata leo! | Jinyoosheni pamoja. Simama wima na ufikie mawingu, inama kuwadia upande mmoja, kisha upande ule mwingine. Rudia. Nyoosheni miili yenu! | Msaidie mtoto wako kujifunza jina lake, anwani na nambari ya simu. | Mfanye mtoto wako akusaidie na kazi moja ya nyumbani leo. | Pulizeni viputo kwa pamoja. Itachukua muda gani kabla ya moja kupasuka? Vinaelea juu mpaka wapi? |
| Ukiwa na mtoto wako, angalia picha katika kitabu na ukisie ni nini kitakachofanyika. Kisha kisome ili kuona kama uko sahihi! | Tembelea maktaba ili kuchagua vitabu na mtoto wako. Msaidie mtoto wako kujifunza kuuliza mwangalizi wa maktaba kwa mapendekezo au eneo maalum la kitu kimoja. | Cheza Mchezo wa Nambari: andika nambari kwenye kijia cha kutembea nje kisha ita nambari hizo na ukimbie kwenye nambari hizo. | Cheza "Taa Nyekundu, Taa ya Kijani" | Tembelea mahali katika jamii yako ambapo hujawahi kufika bado. | Uliza mtoto wako ni nini kinachomsumbua. | Fikiria vitu 5 ambavyo vina rangi ya machungwa. Fikiria vitu 5 vilivyo dukani. Fikiria vitu 5 ambavyo ni laini. |
| Soma kitabu kuhusu wanyama. Je, ni mnyama upi unayempenda sana? | **R** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/mchore **R** mkiwa pamoja. Tafuta "**R**" leo au vitu ambavyo vinaanza na sauti ya /r/ kama vile *ramani*. | Leo ni siku ya rangi ya **kahawia**. Angalia ni vitu vingapi vyenye rangi ya **kahawia** unavyoweza kupata. Zungumzia kuhusu ni vitu vingapi vina rangi ya **kahawia**. | Chora picha ya mti katika kila msimu: machipuko, joto, majani kupukutika, baridi. Zungumzia kuhusu majira yanayobadilika. | Kuwa na wakati wa hadithi ya familia leo. Mruhusu kila mwanafamilia kuchagua kitabu akipendacho na kusoma pamoja. | Jifunze kuonyesha nyuso za kukata tamaa kwenye kioo wakati wako wa kulala. | Zungumzia kuhusu upepo mkiwa pamoja. Je, ni vitu gani vinaweza kupulizwa na upepo? Unaweza kujaribu ubashiri wako kwa kutumia feni? |

## KUCHEZA NA VIDOLE: Five Plump Peas

**Five plump peas in a pea pod pressed.** *(Shikilia ngumi moja juu)*
**Moja ilikua, mbili zikakua, na hata zile zingine.** *(Fungua ngumi-kidole kimoja baada ya kingine)*
**They grew and they grew and they never stopped.**
*(Ukianza mikono ikiwa pamoja, itanganishe ili kila moja "ikue")*
**They grew so big that the pea pod popped!** *(Piga makofi baada ya "popped")*



# JIFUNZE HESABU KILA SIKU

Hesabu haihusu tu kuhesabu na nambari. Kuna njia nyingi za kujumuisha hesabu katika shughuli za kila siku za mtoto wako.

- **WATOTO WACHANGA:** Tumia shughuli za kila siku kama nafasi ya kuhesabu. Hesabu soksi unapokuwa ukizivalisha mtoto wako, hesabu vidole vya mguu vya mtoto, mwambie wapi unapoweka vitu ("ninaweka bloku juu ya mnara").
- **WATOTO WADOGO:** wanaweza kuanza kutambua maumbo, kupanga vitu kwa aina na kutumia maneno ya nambari. Kukariri mashairi yenye vina na kuimba nyimbo ambazo zinajumuisha maneno ya nambari na mtoto wako.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** wanaweza kutatua matatizo ya hesabu ya kila siku, kama vile ni sahani ngapi za kupanga mezani wakati wa chakula cha jioni. Wanaweza kutambua na kutengeneza ruwaza, na kuhesabu mpaka 10 au zaidi kwa sauti. Kusoma vitabu ambavyo vina dhana za hesabu.

# SEPTEMBA

**RASILIMALI ZA NDANI:** Kuna mambo mengi ya familia kufanya katika Kaunti ya Ingham, hakuna kalenda inayoweza kuorodhesha mambo haya yote! Kwa matukio ya burudani ya familia, tembelea Hulafrog kwenye www.hulafrog.com. Ili kujua zaidi kuhusu rasilimali na matukio yanayohusiana na mwaka wa kupata mtoto na familia zenye watoto wadogo, tembelea Willow Tree Family Center kwenye www.willowtreefamily.com.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Sema matamanio kwenye nyota pamoja usiku. Elezeaneni matamanio yenu. | **S** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore **S** mkiwa pamoja. Tafuta "**S**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /s/ kama vile *sabuni*. | **Mstatili** ndio umbo la siku ya leo. Hesabu ni **mistatili** ngapi unaweza kupata leo! | Tembelea maktaba ukiwa na mtoto wako wiki hii. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. Tembelea matukio: *www.cadl.org/events* au *www.elpl.org*. | Choreni ramani ya mtaa wenu pamoja. Zungumza na mtoto wako kuhusu mahali vitu vilipo. | Chora uso wenye hasira na uzungumzie kuhusu wakati ulikuwa umekasirika. | Cheza mchezo wa kufuata maelekezo, kama vile "Simon Asema" na mtoto wako. |
| Himiza mtoto wako kukusimulia hadithi. Andika anachokisema na umsomee hadithi hiyo wakati wa kulala. | Pamoja na mtoto wako fikiria kuhusu vitu 10 vifanyavyo vina na neno "hasira". | Leo tunashughulikia nambari **9**. Angalia ni **9** ngapi unazoweza kupata unapokuwa ukiendelea na shughuli zako za siku. | Tengeneza ndege ya karatasi na ipeperushe pamoja. | Tembelea sehemu ya watoto ya maktaba ya eneo lako. | Lala chini na ufunge macho yako. Je, unaweza kujiskia ukipumua? Unaweza kusikia moyo wako ukidunda? Je, umetulia? | Jadili mzunguko wa maisha ya mmea: mbeguchipuko, mti. Chora kila hatua kwenye kadi ya faharasa. Msaidie mtoto wako kuziweka katika mpangilio sahihi. |
| Imba na uigize wimbo, "The Wheels on the Bus." | **T** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore **T** mkiwa pamoja. Tafuta "**T**" leo au vitu ambavyo vinaanza na sauti ya /t/ kama vile taa. | Leo ni siku ya rangi **nyeusi**. Angalia ni vitu vingapi vyenye rangi **nyeusi** unavyoweza kupata leo. Zungumzia kuhusu vitu ambavyo ni **nyeusi**. | Tafuta baadhi ya vitu unavyoweza kufuatisha. Mruhusu mtoto wako avifuatishe na kisha ajaribu kulinganisha vitu hiyo na umbo lake. | Kaa chini na kula pamoja, zungumzeni kuhusu shughuli yako uipendayo ya majira ya majani kupukutika. | Tengeneza kitabu cha hisia kwa kutumia karatasi iliyokunjwa. Chora nyuso zinazoonyesha hisia tofauti. Ziweke lebo mkijadili hisia na mtoto wako. | Tengenezeni matope nje. Inakuwaje ukiweka maji kwenye mchanga kavu? |
| Imba wimbo wa ABC kwa kutumia sauti za ucheshi—roboti, dinosoria, n.k. | Unapokuwa ukisoma hadithi na mtoto wako, uliza maswali ya "ni nani," "ni nini," "ni wapi," "ni lini" na ni "kwa nini". | Wakati unakula tunda dogo lolote lile au vitafunio vihesabu pamoja. | Jifunze kukata mistatili. | Jifunze kutumia "tafadhali" na "asante" na watu wengine. | Piga rangi au chora kwa kutumia vidole au brashi. Weka muziki na mhimiza mtoto wako kupaka rangi kama anavyohisi ule muziki. | Jifanye wewe ni mpiga picha na upige picha. |
| Zungumzia kuhusu mwezi na uchore picha yake. Je, mwezi una umbo lipi? | Msaidie mtoto wako kuandika jina lake kwa kutumia unga wa kuchezea, chumvi, krimu ya kunyolea, kalamu ya rangi, n.k. | Tambua nambari kwenye simu. Zungumzia kuhusu nambari yako ya simu na ujaribu kuikumbuka. Tunga wimbo kuhusu nambari yako ya simu. | Jifunze kuruka, kutambaa au kuruka vitu vilivyo nje. | Andika barua au chora picha kwa rafiki mpya. | Mfanye mtoto wako ajifunze kuvaa koti yake mwenyewe na kubeba mfuko wake. | Bashiri ni nini kitakachozama au kuelea kwenye karai ya bafu au karo. |

**WIMBO:**
**Wheels on the Bus**

The wheels on the bus go round and round,
Round and round, round and round.
The wheels on the bus go round and round,
All through the town.

The wipers on the bus go swish, swish, swish…
The driver on the bus says "move on back"…
The people on the bus go up and down…
The babies on the bus go "wah, wah, wah"…
The parents on the bus say "I love you, I love you, I love you"…

# SANAA YA KILA SIKU

## BUNI, CHUNGUZA, FIKIRIA!



Kutengeneza sanaa hujenga umahiri  wa misuli, huimarisha kujiamini na huwawezesha watoto kushiriki hisia zao kwa njia inayofaa kwa umri wao. Sanaa huboresha ujuzi wa juu wa kufikiria wa mtoto na kuwahimiza kutumia ubunifu wao. Tengeneza nafasi ambayo ni sawa kuchafua.

- **WATOTO WACHANGA:** Waruhusu kuchunguza unamu tofauti ambao ni salama kugusa na kuonja, hata wakati wa kula. Waruhusu wararue barua taka!
- **WATOTO WADOGO:** Anza kwa urahisi! Hauhitaji vifaa maridadi vya sanaa—tumia penseli, kalamu za watoto, krayoni, karatasi zisizotumika. Waruhusu wajifunze na vifaa. Epuka kutoa maelekezo au kupendekeza mabadiliko. Kumbuka mchakato wa kubuni ni muhimu zaidi kuliko matokeo yake.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** Uliza mtoto wako akuambie kuhusu kazi yake ya sanaa. Tafuta nafasi  ya kuonyesha kazi yake ya sanaa. Kama badohujafanya hivyo, ongeza vifaa zaidi kama vile rangi ya maji, gundi na makasi yasio na ncha kali ili kukata karatasi.

# OKTOBA

**RASILIMALI ZA NDANI:** Jumba la makumbusho la Eli and Edythe Broad Art Museum hutoa Siku za Familia kila jumamosi ya kwanza ya kila mwezi (isipokuwa siku za wikendi), kuanzia saa 5 asubuhi – 9 mchana. Familia zenye watoto wa umri wote zinaweza kufurahia kutengeneza sanaa. 547 E Circle Dr., East Lansing, MI 48824, *www.broadmuseum.msu.edu.*

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Toa CD au albamu ya hoopla kutoka kwenye maktaba na ujifunze wimbo mpya pamoja. | Soma na mtoto wako anapokuwa akioga. Utapata hadhira tekwa na mtoto wako atafurahia mshangao huo! | Umbo la siku ni **duara**. Hesabu ni **miduara** mingapi unaweza kuona leo! | Chora picha mkiwa pamoja. Lenga mchakato na furaha ya kuchora, sio matokeo yenyewe. | Tembelea maktaba ukiwa na mtoto wako wiki hii. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. Tembelea matukio: *www.cadl.org/events* au *www.elpl.org*. | Jifunze kunawa mikono, kusugua meno na kuchana nywele. | Tengeneza msuguo wa majani. Kusanya majani, yaweke chini ya karatasi, na usugue krayoni kwenye karatasi. Unamu na maumbo ya burudani! |
| Mfanye mtoto wako aoshe mtoto wake sesere. Zungumzia kuhusu kila hatua ya mchakato huu. | **U** ni herufi ya leo. Fuatisheni/mchore **U** mkiwa pamoja. Tafuta "**U**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /u/ kama vile *uso*. | Kusanya mawe 10. Je, zinafanana aje? Zinatofautiana aje? | Muache mtoto wako akusaidie kusomba majani. Ruka, kimbia, rusha majani na mcheze pamoja! | Msaidie mtoto wako kumpigia simu rafiki yake au ndugu maalum ili kumwambie mambo mawili kuhusu majira ya majani kupukutika. | Jifanye wewe ni mtoto na umruhusu mtoto wako awe mzazi. Waruhusu wafurahie kukushughulikia! | Tembea pamoja. Kusanya vitu vya asili kutoka ardhini. Tumia mkusanyiko wako kutengeneza sanaa ya majani. Soma *Leaf Man* ya Lois Ehlert. |
| Piga kambi nje! Tengeneza ngome kwa kutumia viti na blanketi. Mfanye mtoto wako abuni hadithi na wewe kuhusu kupiga kambi. | Soma kitabu cha maelezo kuhusu Msimu wa majani kupukutika leo. Zungumzia kuhusu ni kwa nini majani hubadilika na aina gani ya matukio tunayofurahia katika msimu wa majani kupukutika. | Leo tunashughulikia nambari **10**. Je, ni **10** ngapi unazoweza kupata leo? Hesabu vitu kwa **10** ikiwa unaweza! | Mfanye mtoto wako aweke vibandiko kwenye karatasi. Vibandiko hivyo vinaweza kuwa kitu chochote. Watoto wanapenda kukuza umahiri wa misuli kwa kutumia vibandiko! | Kaa chini na  kula pamoja. Mweleze mtoto wako kuhusu siku yako na muulize kuhusu ya kwake. | Zungumza na mtoto wako kuhusu vitu vya msimu unavyoviona dukani na hisia vinavyokupa. Ni nini ya kweli na kujisingizia? | Kusanya na ukunje majani kavu nje. Je, yanatoa sauti gani? Je, yanatoa harufu gani au yanasikiajie? Weka majani chini ya karatasi, na usugue krayoni juu ya karatasi. |
| Tafuta picha ya familia yako. Zungumzia kuhusu familia yako na nini huwafanya wawe maalum. | Weka krimu ya kiasi ya kunyolea kwenye sinia au karai ya bafu. Jifunze kuandika jina la mtoto, herufi, umri wao, na nambari. | Fikiria vitu 5 ambavyo ni vidogo. Fikiria vitu 5 ambavyo vina rangi ya zambarau. Fikiria kuhusu wanyama 5. | **V** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore **V** mkiwa pamoja. Tafuta "**V**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /v/ kama vile *vazi*. | Tembelea bustani ya mboga au Soko la Wakulima na mzungumzie kuhusu shughuli za  mkulima. | Chora uso wa kutisha na uzungumzie mambo ambayo yanatisha. | Chonga boga au andaa boga. Mruhusu mtoto wako kusonga mbegu zilizo ndani kwa mikono yake na mhesabu mbegu pamoja! |
| Tembeeni nje na mzungumzie kuhusu mabadiliko mnayoyaona katika msimu wa majani kupukutika. | Tengeneza kadi yako mwenyewe ya salamu. Tengeneza kadhaa ili uwe nazo wakati hafla inapotokea. | Tengenezeni ruwaza pamoja. Badilisha rangi tofauti za soksi. Je, ni nini hufuatilia katika ruwaza? | Tengeneza utando wa buibui kwenye sakafu kwa kutumia utepe au uzi. Jifanye nyie ni buibui. | Cheza mchezo pamoja (Peek-a-Boo, Hide & Seek, I Spy, n.k.). | Sema "tafadhali" na "asante" mara kwa mara—mtoto wako atafanya hivyo pia. | Jaribu ili kuona ni vitu gani vinavyoelea au kuzama bafuni. |

**WIMBO:**
**Piga Makofi**

Clap your hands, clap your hands, clap them just like me.
Touch your ears, touch your ears, touch them just like me.
Tap your feet, tap your feet, tap them just like me.
Pat your head, pat your head, pat it just like me.



# KUANDIKA HUANZA
## MAPEMA KABLA YA WATOTO WAWEZA KUSHIKILIA PENSELI

Watoto wanahitaji fursa ya kukuza ushirikiano wa macho na mkono, na kuelewa kwamba mawazo yanaweza kuandikwa na kusomwa na wengine.

- **WATOTO WACHANGA:** Wakati wa chakula waruhusu kuchuna, kutoboa na kuchukua vipande vidogo vya chakula. Wape krayoni ili wajifunze kuchora.
- **WATOTO WADOGO:** Wape penseli na vitia alama vinavyoweza kuoshwa ili waweze kujifunza kuchora na kupaka rangi. Wasaidie kutumia vidole vyao kuchora kwenye mchanga. Waruhusu kuchana karatasi, kisha kuunganisha vipande pamoja. Tengeneza unga wa kuchezea ili waweza kuubiringiza, kuupasuka na kukata.
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** wanaweza kuanza kuandika maneno ya kawaida kama vile majina yao. Toboa mashimo kwenye karatasi ngumu na wape kamba ya kiatu ili kuipitisha kwenye mashimo. Wape vibandiko vya kuweka kwenye karatasi. Msaidie mtoto wako kuweka kichwa kwenye kazi yake ya sanaa au atoe imla ya hadithi ili uweze kuiandika. Andikeni pamoja orodha ya mahitaji kwenye karatasi na itumie wakati wa kununua.

# NOVEMBA

**RASILIMALI ZA NDANI:** Muda wa hadithi wa maktaba hutoa nafasi ya kuandika na baadhi ya maktaba yana kituo cha mwandishi. Tafuta maelezo kwenye *www.cadl.org* au *www.elpl.org*.

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Cheza "mchezo wa kinyume." Sema neno na umfanye mtoto wako akuambie kinyume chake. | **W** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore **W** mkiwa pamoja. Tafuta "**W**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /w/ kama vile *wali*. | Umbo la leo ni **umbo la yai**. Hesabu ni **umbo la yai** ngapi unaweza kupata leo. | Chagua nambari ya leo. Angalia ni vitu vingapi unaweza kupata ambavyo vilikuja katika nambari hiyo. Angalia kama unaweza kupata nambari hiyo katika chapa. | Hesabu nambari ya ngazi unapokua ukimsaidia mtoto wako kupanda au kuteremka. | Badilisheni majukumu. Jifanye kuwa mtoto wakati mtoto wako anakushughulikia. | Tengeneza matandiko ya meza kwa ajili ya wakati wa kula. Si lazima wawe wazuri sana. |
| Tengeneza vikaragosi kwa kutumia mifuko ya karatasi ya rangi ya kahawia. Kwa pamoja, toa hadithi kwa kutumia vikaragosi vyako. | Buni hadithi pamoja. Chukueni zamu kuongezea zaidi kwenye hadithi. Iandike. | Msaidie mtoto wako kuandaa meza. Amua ni wapi kila mtu ataketi. | Imba: "Piga makofi 1, 2, 3. Piga makofi kama mimi." (Kisha kunja, punga, n.k.) | Tembea au tembelea kituo cha mambo ya asili cha eneo lako na utafute wanyama. | Zungumzia kuhusu jinsi sisi sote ni wa kipekee na maalum. Mfanye mtoto wako ataje baadhi ya mambo maalum kuhusu wao wenyewe. | Tengeneza darubini kutoka kwenye tyubu za kadibodi zilizounganishwa pamoja. Cheza "I Spy" au kuwa mchunguzaji! |
| Mfanye mtoto wako akusaidie kutengeneza orodha ya vitabu, nyimbo, marafiki zake awapendao, n.k. Hifadhi orodha hiyo ili aiangalie tena akikua mkubwa zaidi. | Andika barua kwa mwanafamilia leo. | Cheza na maharagwe au pasta kavu katika kikaangio au blanketi. Ipitishie magari ya kuchezea kwayo, ichote, imwage kwa kutumia vikombe vya kupimia. | **X** ndio herufi ya leo. Fuatisheni/ mchore **X** mkiwa pamoja. Tafuta leo "**X**" au vitu vinavyoisha na sauti ya /x/ kama vile *box*. | Hudhuria wakati wa hadithi katika maktaba na mtoto wako wiki hii. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. Tembelea matukio: *www.cadl.org/events* au *www.elpl.org* | Chora picha za kibinafsi na mtoto wako. Zizungumzie pamoja. | Mpe mtoto wako pasta kavu na gundi na umruhusu kutengeneza kolagi kwenye kipande cha karatasi. |
| Jifunze wimbo wa mwezi huu. | Tembelea maktaba ukiwa na mtoto wako wiki hii. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. Tembelea matukio: *www.cadl.org/events* au *www.elpl.org* | Chora pai kwenye sahani. Kisha ikate kwa nusu na robo. | Chora nje ya mkono wako na kisha upambe kwa kutumia krayoni, kalamu za rangi au rangi. | Tengenezeni pamoja orodha ya shukurani. Fanya kila mmoja wa familia yako ataje kitu ambacho anashukuru. | Mfundishe mtoto wako njia sahihi ya kunawa mikono yake. Tunga wimbo ili kumsaidia kuendelea kunawa mikono kwa muda sahihi. | Zungumzia leo kuhusu familia. Inamaanisha nini kwako? Ni nani ako katika familia yako? Chora picha au andika hadithi. |
| Rangi ya leo ni **kijivu**. Angalia ni vitu vingani vina rangi ya **kijivu** unavyoweza kupata leo. Zungumzia kuhusu rangi ya **kijivu**. | Unapokuwa ukitembea au kuendesha gari, taja ishara unazoona au hesabu ni ishara gani ambazo mtoto wako hutambua (ishara za kusimama, duka la mboga, mikahawa, n.k.). | Fuatilia mguu wa mtoto wako kwa kalamu na mkate pamoja mchoro huo. Pima vitu nyumbani kwa kutumia "futi". Mtoto wako ana urefu wa "futi" ngapi? | Jifunze kutambaa, kuruka au kurukia vitu nyumbani. | Kuwa na wakati wa hadithi ya familia leo. Mfanye kila mwanafamilia amechagua hadithi aipendayo na msome pamoja. | Likizo zinaweza kuwa za kusumbua. Jifunze kupuliza viputo ili kushughulikia kupumua ili kujituliza. | Kucheza kwa kutumia unga wa kuchezea kunaweza kuwa shughuli ya kutuliza. Tengenezeni pamoja, kisha toboa, pasua, finya na uiponde ukizungumzia kuhusu njia za kujisaidia kutulia. |

**WIMBO:**
**If You're Happy and You Know It**

If you're happy and you know it clap your hands.
If you're happy and you know it clap your hands.
If you're happy and you know it then your face will surely show it,
If you're happy and you know it clap your hands.
*(Pia jaribu "kutingiza kichwa chako," "gonganisha miguu yako," na "fanya zote tatu.")*



# WEKA AKIBA, TUMIA, TOA

Kuanzisha uwajibikaji na usimamizi wa pesa mapema kutasaidia mtoto wako kukua na kuwa mtu mzima anayewajibika kifedha.

- **WATOTO WACHANGA:** Anzisha dhana ya kuweka akiba, kutumia, na kutoa na "Chupa ya Akiba" ya pesa za zawadi au salio ndogo. Anzisha dhana ya jinsi ya kufanya maamuzi kuhusu kushiriki na kutumia pesa wakati wamekuwa tayari kuweza kuelewa.
- **WATOTO WADOGO:** Msaidie mtoto wako kujifunza kuchukua zamu, na uonyeshe kuwa utulivu wewe mwenyewe kwa kuwa mtulivu ukisubiri mwenendo wa magari au kwenye foleni dukani. Utulivu ni sehemu muhimu ya kuweka akiba pesa!
- **WATOTO WA CHEKECHEA:** Anzisha misingi ya kifedha kwa kumsaidia mtoto wako kujifunza kutaja na kupanga pesa. Watie moyo kucheza "Duka," na uwape kazi ndogo wakati mnanunua kwa pamoja, kama vile kutafuta bidhaa kwenye orodha au kumpa keshia pesa.

# DESEMBA

**RASILIMALI ZA NDANI:** CACS Head Start hutoa masomo ya Usimamizi wa Pesa kwa familia katika jamii. Elimu ya Kifedha ya MSUFCU hushiriki pamoja na shule ya kienyeji, mashirika, vyama, na washirika wengine wa jamii ili kutoa maonyesho, matukio na shughuli za elimu. Tembelea *www.cacsheadstart.org/Family-Services* na *www.msufcu.org/events.*

| JUMAPILI | JUMATATU | JUMANNE | JUMATANO | ALHAMISI | IJUMAA | JUMAMOSI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jifanye unazungumza kwenye simu na mtoto wako. Kuongea huongezea misamiati ambayo huwasaidia watoto kuwa tayari kusoma! | **Y** ndio herufi ya siku. Fuatisheni/ mchore **Y** pamoja. Tafuta "**Y**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /y/ kama vile *yai.* | Andika nambari 1–5 kwenye karatasi. Kando ya kila nambari, chora vitu vya kutafuta. (mpira-1, soksi-2, bloku-3, n.k.) | Kuchana karatasi. Mruhusu mtoto wako kukuza umahiri wa misuli kwa kuraruchana karatasi. Unganisha karatasi hiyo ili kuwa kolagi, ifaavyo. | Zungumzia kuhusu rangi zako uzipendazo. Tembea leo na utafute rangi hizo kila mahali! | Chukueni zamu kufanya nyuso kwenye kioo. Onyesha furaha na uzungumzie kuhusu vitu vinavyofurahisha. | Kusanya vitu nyumbani. Zipange kwa ukubwa: ndogo, wastani, kubwa, ndogo zaidi, n.k. au kwa rangi. |
| Zungumzia kuhusu siku yako. Je, ulifanya nini? Ilikuwaje? Uliona nani? Ulikula chakula gani mchana? | Cheza mchezo wa mashairi ya vina! Sema neno na kisha himiza mtoto wako kusema neno lingine neno lifanyalo kina. | Tengenezeni ruwaza pamoja. Badilisha kati ya rangi tofauti za vitu. Je, ni nini hufuatilia katika ruwaza? | Cheza "Follow the Leader." | Cheza mchezo wa kukisia. Fafanua kitu na uone kama unaweza kukisia ni nini. Kisha mruhusu mtoto wako kufafanua kitu. | Ruhusu mtoto wako kuchukua maamuzi, kama vile ni soksi gani ya kuvaa. Kuchukua maamuzi hujenga uwezo wa kujitegemea na ujasiri. | Buni kitu kwa kutumia vitu vinavyoweza kutumika tena kama vile visanduku, karatasi au chupa za plastiki. |
| Zungumzia kuhusu shughuli za wanyama katika msimu wa baridi. | **Z** ndio herufi ya siku. Fuatisheni/ mchore **Z** kwa pamoja. Tafuta leo "**Z**" au vitu vinavyoanza na sauti ya /z/ kama vile ***zambarau.*** | Tafuta leo mitindo katika mazingira (kwenye zulia, kwenye dari, unapotembea kwenye majengo, n.k.). Yazungumzie kwa pamoja. | Cheza muziki au piga makofi na kisha usitishe na "usimame tuli." Haya ni mazoezi mazuri ya kusikiliza na kutoyumba! | Mruhusu mtoto wako kutoa imla ya barua ili uweze kuandika. Muonyeshe maneno yake na msaidie kufikisha barua hiyo kwa mtu maalum. | Furahia kucheza na mtoto wako kwa dakika 20. Mwache aongoze. | Tengeneza biskuti na uzishiriki na familia au marafiki. |
| Zungumzia kuhusu msimu wa baridi huko Michigan na duniani kote leo. Je, kuna baridi kila mahali? | Tafuta picha za dubu (au vitu vingine) katika kitabu pamoja. Hesabu ni ngapi unazopata. | Zoeza kuhesabu za kinyumenyume kuanzia 10. | Jifanye kuwa vipande vya theluji, kisha mipira ya theluji, kisha mtu wa theluji, na kisha myeyuke pamoja. | Cheza "Mimi Napeleleza." Sema, "Mimi napeleleza kitu cha duara na njano." Uone kama mtoto wako anaweza kukisia ni nini. | Mpongeze mtoto wako kwa kufanya kitu vizuri; sema ni nini hasa. | Jifunze kuvaa nguo na kuvua nguo kwa hali baridi ya hewa. |
| Zungumzia kuhusu marafiki leo. Inamaanisha nini kuwa rafiki mzuri? | Tembelea maktaba ukiwa na mtoto wako wiki hii. Chagua vitabu au usalie na usome kwa muda. | Umbo la leo ni **almasi**. Hesabu ni **almasi** ngapi unaweza kupata leo! | Nenda nje na mzungumzie kuhusu msimu wa baridi unafananaje. Je, kuna theluji? | Zungumzia leo kuhusu kutoa zawadi. Tengeneza zawadi wenyewe kwa mtu unayempenda. | Chora picha pamoja, ukizingatia mchakato, si matokeo yake. Zungumzia kuhusu kile kila mmoja wenu anakichora. | Choreni pamoja mtu wa theluji. Zungumzia kuhusu vifaa vya ziada kwa ajili ya mtu wako wa theluji. Je, anapaswa kuvaa kofia ya rangi gani? |

**WIMBO:**
**Twinkle, Twinkle, Little Star**

Twinkle, twinkle, little star
How I wonder what you are.
Up above the world so high,
Like a diamond in the sky,
Twinkle, twinkle, little star
How I wonder what you are.

# JINSI WATOTO WALIVYO: Kuzaliwa hadi Umri wa miaka 5

Imetolewa kwa: "TOYS: Tools for Learning." Brosha ya NAEYC #571

Watoto wawili hawaendi sambamba wakikua. Hapa kuna baadhi ya mambo unayoweza kutafuta unapokuwa ukiona mtoto wako akikua. Ikiwa una maswali au wasiwasi kuhusu jinsi mtoto wako anavyokua, huenda ukataka kuongea na daktari wa mtoto wako au piga simu bila malipo kwa nambari zilizoorodheshwa hapa chini.



| UMRI WA KUKADIRIA | JINSI WATOTO WALIVYO |
|---|---|
| **KUZALIWA HADI MIEZI 3** | Huanza kutabasamu, kulia polepole<br>Hufuata mtu au kitu kinachosonga kwa macho<br>Hupendelea nyuso na rangi ang'avu<br>Hufikia, kugundua mikono, kurusha mateke, kuinua kichwa<br>Kunyonya kwa kufurahia<br>Hulia, lakini mara kwa mara hutulia akibebwa<br>Hupindua kichwa kuwadia sauti |
| **MIEZI 4 HADI 6** | Hupendelea wazazi na ndugu wakubwa zaidi ya watu wengine<br>Hurudia vitendo vyenye matokeo ya kuvutia<br>Husikiliza kwa makini, na kuitikia akizungumziwa<br>Hucheka, kugugumia, kuiga sauti<br>Huchunguza mikono na miguu, huweka vitu mdomoni<br>Hukaa akikalishwa chini, hupinduka, huenda mbio, kuruka<br>Hushika vitu bila kutumia vidole gumba, hugonga vitu vinavyoning'inia<br>Hutabasamu mara kwa mara |
| **MIEZI 7 HADI 12** | Hukumbuka matukio za kawaida, hutunga dhana rahisi<br>Hujitambua, hutambua sehemu za mwili, na sauti za watu anaowafahamu<br>Huelewa jina lake mwenyewe, maneno mengine ya kawaida<br>Husema maneno ya kwanza muhimu<br>Huchunguza, kugonga, au kutikisa vitu na mikono<br>Hutafuta vitu vilivyofichwa, huweka vitu ndani na nje ya kontena<br>Hukaa peke yake<br>Hutambaa, kujisimamisha, kusimama, kutembea<br>Huenda akaonekana lkuwa mwoga au kukasirishwa na wageni |
| **MWAKA 1 HADI 1½** | Huiga hatua za watu wazima<br>Huongea na kuelewa maneno na dhana zaidi<br>Hufurahia hadithi<br>Hujaribu na vitu<br>Husimama wima, hupanga ngazi<br>Huonyesha kujitegemea, lakini hupendelea watu ambao anawafahamu<br>Hugundua kumiliki vitu<br>Hupata marafiki, lakini pia hucheza peke yake<br>Huanza kuelewa watu wazima wanataka afanye nini, lakini bado hana uwezo wa kujidhibiti |
| **MIAKA 1½ HADI 2** | Hutatua matatizo<br>Huongea na kuelewa hata zaidi<br>Huonyesha kujivunia kutimizia kitu, kama vile kusaidia na kazi<br>Huonyesha kudhibiti mwili zaidi, kukimbia<br>Hucheza zaidi na wengine<br>Huanza kucheza kwa kujifanya |
| **MIAKA 2 HADI 3½** | Hufurahia kujifunza ujuzi mpya<br>Hujifunza lugha kwa haraka<br>Daima wanajishughulika<br>Huanza kufahamu hatari<br>Hupata udhibiti zaidi wa mikono na vidole<br>Hukasirishwa haraka<br>Hutenda kwa njia ya kujitegemea zaidi, lakini bado anategemea wengine pia |
| **MIAKA 3½ MIAKA 5** | Huiga matukio ya kawaida<br>NI mwangalifu kwa muda mrefu zaidi<br>Hutenda kiupuuzi, hujigamba, anaweza kutumia lugha ya kushtua<br>Huongea sana, huuliza maswali mengi<br>Anataka vitu vya kweli vya watu wazima, huhifadhi miradi ya sanaa<br>Hujaribu ujuzi wa kimwili na ujasiri kwa uangalifu<br>Huonyesha hisia katika michezo ya kuigiza<br>Anapenda kucheza na marafiki, hapendi kushindwa<br>Hushiriki na kuchukua zamu wakati mwingine |

early on MICHIGAN

Kwa msaada na maelezo bila malipo kwa watoto kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 3 na labda wanaochelewa kukua au walemavu. Piga simu bila malipo kwa 1-800-EarlyOn (1-800-327-5966) au tembelea *www.1800EarlyOn.org*

build up
MI Kids. Kindergarten Ready.

Build Up huwasaidia wazazi na watoto wao, wenye umri wa miaka 3 hadi 5 ambao wanapata shida kusoma na labda wanahitaji usaidizi na/au huduma za elimu maalum. Piga simu bila malipo 1-800-320-8384 au tembelea *www.BuildUpMi.org* kwa maelezo zaidi.

# KUSOMA UKIWA SHUGHULINI

## NYUMBANI:

Unaweza kubadilisha kazi na shughuli za kila siku za nyumbani kuwa michezo ya kusoma ya burudani kwa mtoto wako.

### Kufua Nguo

Shughuli za kufua nguo zinaweza kuunda ujuzi wa hesabu na kushirikiana. Vilevile kuhisi kama unafaa inawasaidia watoto kuhisi vizuri, na huwahimiza kuendelea kutaka kusaidia. Mtoto wako anaweza:

- Kutengeneza mafungu ya nguo nyeupe na nguo nyeusi.
- Kupata soksi zinazolingana.
- Kupata mashati zote ya kuweka kwenye fungu ili kuzikunja.

### Wakati wa Kula

Majadiliano mezani yanaweza kumsaidia mtoto wako kukua na kukuza kujifunza. Maingiliano wakati wa kula huwasaidia watoto kutumia lugha kuchanganua, kufuatilia na kubashiri na kukuza upendo wa lugha.

- Uliza mtoto wako akueleze hadithi kuhusu siku yake au mwambie hadithi kuhusu siku yako.
- Mruhusu mtoto wako akusaidie kuandaa chakula—chana saladi, koroga mchuzi wa tambi, au kusaidia kuandaa meza.

### Wakati wa Kulala

Msaidie mtoto wako kupumzika mwisho wa siku na ufanye wakati wa kulala kuwa wenye amani na utulivu zaidi.

- Unda ratiba thabiti ya wakati wa kulala ambayo mtoto wako anaweza kutegemea.
- Kwa mfano: Kuoga, kupiga mswaki, kusoma hadithi, kumpa busu, kwenda kulala.
- Mtoto wako wa chekechea anaweza kusaidia kupanga ratiba ya wakati wa kulala na kutumia muda maalum wa kusikiliza hadithi, kubuni hadithi, au kuzungumzia siku.



## KUSAFIRI:

Tumia wakati wa kusafiri kuboresha hamu ya mtoto wako ya vitu asilia na utafute njia za kutangamana na kupatana na mtoto wako.

### Ndani ya Gari/Basi

- Zungumzia kuhusu siku ya mtoto wako. Uliza maswali maalum: "Je, ulichora huko chekechea?" au "Ulikula sandwichi ya jibini?"
- Ongea na mtoto wako kuhusu mahali unapoenda baadaye ili kumsaidia kukuza ujuzi wake wa kufikiria na kupanga ("Kabla ya kurudi nyumbani, tutasimama njiani huko sokoni").

### Matembezi

- Kumpeleka mtoto wako kutembea si mazoezi mazuri tu, bali humruhusu kuzoea mambo ya asili na kujifunza kuhusu nje.
- Tunga mashairi au imba mnapokuwa mkitembea. Jaribu kutembea na kuimba au kuimba kwa haraka, kisha polepole.
- Msaidie mtoto wako kujifunza kuwa salama kwa kusimama kwenye kona na njia za magari na kumwonyesha kuangalia magari kwa pande zote.
- Uliza mtoto wako maswali. Ni sauti gani unazosikia? Ni wanyama gani unaowaona? Hali ya hewa ikoje leo?

## MAENEO YA UMMA:

### Katika Duka la Mboga

Jitahidi kuhakikishha safari zako kwenda duka la mboga ziwe na elimu na bila taabu.

- Mruhusu mtoto wako kuchagua chakula. Je, tununue tofaa, machungwa, au zabibu leo?
- Mfanye mtoto wako atafute vitu kwenye orodha ya mahitaji.
- Mruhusu mtoto wako kusaidia kupanga bidhaa kwenye maboksi na makopo mkifika nyumbani.

### Katika Bustani/Uwanja wa kucheza

Gundua njia za kubadilisha shughuli ziwe za kusoma.

- Utachukua muda gani kukimbia kuelekea huo mti mkubwa?
- Je, mtelezo gani ni mkubwa zaidi, ule nyekundu au ule wa rangi ya fedha?
- Mfanye mtoto wako ahesabu nambari ya bembea au watoto wengine.

### Katika Maktaba

Maktaba inatoa fursa nyingi za kusoma na ni maeneo ya ajabu ya kuchunguza lugha na vitabu.

- Tembelea maktaba ili upate kadi yako mwenyewe ya maktaba.
- Mruhusu mtoto wako kuchagua vitabu vyao vya maktaba mwenyewe.
- Mfundishe mtoto wako kuhusu kutunza vitabu vizuri na kuazima na kurejesha vitabu.
- Hudhuria wakati wa hadithi na matukio mengine katika maktaba ya eneo lako.



Chanzo: *Born Learning by Mind in the Making*, mradi wa Families and Work Institute. Kwa maelezo zaidi kuhusu vidokezo vya masomo ya mapema kwa wazazi, tembelea *www.bornlearning.org.*

Vidokezo vya masomo ya mapema ya sayansi ya akili: *www.joinvroom.org*
NAEYC kwa familia: *families.naeyc.org*
Ingham Intermediate School District's Family Learning Connection: *www.inghamisd.org/flc*

# WADHAMINI

Capital Area District Libraries

ELPL East Lansing Public Library

Michigan State University Federal Credit Union
Building Dreams Together

# EARLY LEARNING CALENDAR WORKGROUP,

a subgroup of the Ingham School Readiness Advisory Committee

Wendy Boyce, Ingham Intermediate School District
Kim Fiebernitz , Ingham Intermediate School District
Laurie Linscott, Michigan State University Child Development Laboratories
Jennifer McCaffrey, Ingham Intermediate School District
Corrie Mervyn, Ingham Intermediate School District
Michelle Nicholson, Ingham Intermediate School District
Thais Rousseau, Capital Area District Libraries
Gloria Sabourin, Spartan Child Development Center
Mary Jo Wegenke, Ingham Intermediate School District
Jamie Yeomans, Mzazi

# ASANTE

Shukrani maalum kwa Maktaba ya Umma ya Kalamazoo kwa msukumo na kibali cha kutumia maudhui kutoka kwa Kalenda ya Masomo ya Mapema ya Kalamazoo.
Shukrani sana kwa Idara ya Elimusoko ya Maktaba ya Wilaya ya Eneo la Capital kwa mchoro, muundo na mpangilio.